



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA  
THE HANSARD**

Tuesday, 1<sup>st</sup> March, 2023

**Third Assembly – Fifteenth Sitting**

*[The County Assembly met at 10:35a.m. at the County Assembly Buildings]*

*[The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdulkadir) in the Chair]*

**PRAYERS**

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): You may be seated? Yes Clerk?

**MOTION**

MEASURES TO DECONGEST COAST TEACHING AND REFERRAL HOSPITAL

Yes, Honourable Allen Katana MCA Shanzu Ward please move the Motion.

**Hon. Katana:** Mr. Speaker, I beg to move the following Motion:

*THAT AWARE THAT, article 43 (1) (a) of the Constitution of Kenya, 2010 provides that every person has the right to the highest attainable standard of health which includes the right to health care services;*

*FURTHER AWARE THAT, health sector is the biggest function to be devolved under the Constitution of Kenya, 2010 to allow the County government to design innovation models and interventions that suit the unique health needs, encourage effective citizen participation and make autonomous and quick decision on resource mobilization and management;*

*COGNIZANT THAT, the Coast General Teaching and Referral Hospital is the largest public health facility serving the Counties of Mombasa, Kilifi, Lamu, Tana River, Kwale and Taita Taveta;*

*CONCERNED THAT, due to the high number of patients at Coast General Teaching & Referral Hospital the situation has caused congestion, undue delay in service delivery, straining of the available facilities and overworked staff;*

*I, therefore urge this Assembly to RESOLVE;*

1. *THAT, the County government through the Department of Health to conduct a strategic needs assessment survey of the infrastructure, equipment and human resource...*

*[Loud consultations]*

Mr. Speaker, kindly protect me because an Honourable Member is shouting here.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Okay Honourable Juma please remain silent when the Member is on the floor.

**Hon. Katana:** Thank you Mr. Speaker.

1. *THAT, the County government through the Department of Health to conduct a strategic needs assessment survey of the infrastructure, equipment and human resource capacities of all health facilities in the County to be able to know requirement, capacities, for planning and implement solutions accordingly;*

2. *THAT, the County government to upgrade Port Reitz Level 4 Hospital to level 5 and fully equip it to attend to referrals to reduce the overcrowding at the Coast Teaching & Referral Hospital;*

3. *The County government to source for funds for construction of health facilities in every ward and renovate the existing ones for easy access to health care.*

Mr. Speaker, with that I therefore humbly ask the Honourable Chairman for labour Honourable Jacktone Madialo to second. I thank you Mr. Speaker.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Yes Madialo?

**Hon. Madialo:** Mr. Chairman Honourable Katana is a very good friend of mine and it is hard not to support his Motion, I do hereby support.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Thank you. I now propose a question that the Motion by Honourable Allen Katana, on Measures to decongest Coast General Teaching and Referral Hospital to be considered in this Honourable House in the same terms as moved.

*[Question proposed and agreed to]*

Yes, Honourable Allen Katana please make your contribution to the Motion.

**Hon. Katana:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa nafasi hii ulionipa na pia nianze tayari kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Leba Mheshimiwa Madialo. Naamini hajaniunga mkono Mheshimiwa Spika kwa kuwa ni rafiki yangu, lakini ameona hili swala ni la maana sana na ningependa kuzungumzia kiurefu kidogo kuhusu hili swala ambalo liko mbele yetu leo. Mheshimiwa spika kama tujuavyo hospitali yetu kubwa ya Makadara inahudumia kama nilivyo orodhesha hapa, inahudumia Kaunti zote sita za maeneo haya ya pwani.

Hivyo basi, imesababishwa hali ya msongamano ya wagonjwa pale katika kupeana huduma kwa wagonjwa. Mheshimiwa Spika, ningetaka kulitaja hili ya kwamba inafika wakati, nimetembelea pale mgonjwa unaona kabisa hajapona, lakini madaktari kwa kuwa wamempa yale matibabu wanafikiria tayari, huyu ni uzuri apaondoke hapa ili tupate mgonjwa mwingine. Mheshimiwa Spika, sasa inakuwa madaktari pale wako kwa wingi kutafuta idadi ya watu walio wahudumia, lakini sikukuwa na uhakika wa idadi ya wagonjwa; tulio wahudumia wamepata matibabu bora na hivyo basi kwenda nyumbani wakiwa wamepata afueni na tena utakuta nimetaja pale ya kwamba, ni vizuri mapendekezo ya kwamba kila Wadi yenye ina mwakilishi hapa ikaweze kuwa na hospitali ili watu wa pale wakaweze kupata matibabu. Mheshimiwa Spika, sasa ule msongamano ulio pale katika ile hospitali kubwa yetu ya hapa Mombasa ikiwa wagonjwa wamehudumika pale na wamepata yale matibabu ambao hawawezi kuyapata mashinani itakuwa ni vizuri wale wagonjwa badala ya kutolewa pale kupunguza msongamano waende nyumbani, itakuwa ni vizuri watumwe katika hizi hospitali zenye tunaziomba ziwe za Wadi ili wakaendeleo kuangaliwa kwa kina katika zile hospitali ndogo ndogo zilizo pale.

Tena si matibabu tu; Mheshimiwa Spika hizi hospitali zenye ziko mashinani zitakapofanywa kuwa imara, mimi nataka kuamini pia zitaleta ajira na hili nataka kulileta wazi ya kwamba nataka kuishukuru serikali iliyopita ya Mheshimiwa Mstahiki Gavana Hassan Joho aliweza kutengeneza hospitali kubwa sana ambayo ni namba mbili pwani nzima kwa ukubwa wake na kwa mtazamo itakapokuwa iko pale Wadi ya Shanzu na hili nalisema na nataka liende katika rekodi za Bunge hili, ya kwamba bali na kwamba wagonjwa wa kutoka sehemu zengine watapata huduma pale, vile vile hata wafanyikazi katika hizi idara zengine kama za usafi, upishi lazima watoke katika Wadi ya Shanzu la sivyo wacha iwe kwa rekodi leo ya kwamba Shanzu kutakuwa na maandamano makubwa endapo kuna watu wengine watakuja kuchukua ajira ya ile zahanati ambayo iliyo ya maeneo ya Shanzu. Hio ni kusema kwamba hizi hospitali zengine ambazo ziko kwa wadi zingine zitakapo boreshwa, vile vile pia zitawezesha tuwe na ajira katika watu wetu hawa, mbali na kwamba watakuwa nawanapeana huduma kwa wagonjwa, vile vile kutakuwa kumetoka nafasi za ajira kwa watu wetu. Kitu kingine Mheshimiwa Spika ni kwamba tutakapo wezesha ile hospitali yetu ya Port Reitz, kwa sababu ni hospitali ambayo imekuwa kwa mda mrefu, ni hospitali ya kihistoria na bado haijapanda kwa *level* yoyote ya maana, itakapowezeshwa na kuwa level ya nne vile vile nina hakika sana Mheshimiwa Spika itaweza kupunguza ule msongamano ambao tunauona katika hospitali yetu kubwa, kwa hayo mengi naomba nikome hapo Mheshimiwa Spika. Ahsante sana.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Thank you. Yes, Honourable Benard Ogutu make your contribution please.

**Hon. Ogutu:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia hii nafasi, japo bado nilikua najiandaa vizuri. Kwanza kabisa nataka nimpongeze ndugu yangu Allen Katana kwa kuleta hoja hii, kwa wakati huu. Walakin ningependa kum *refer* kwa ile Ripoti ambayo tulileta hapa juzi, katika haya maombi mengi ambayo ameweka tumeweza kuzizingatia katika ile Ripoti ambayo ilipita ndani ya hili Bunge. Tuliweza katika ile Ripoti ku *recommend* kwamba Coast General iwe *autonomous* iwe ina *run* kivyake alafu katika kila *Sub County* iwe na Level 4 Hospital ambayo haitafanya watu wa hapo wafanye *referral* katika *Coast General*, alafu katika kila area tuwe na Level 2 na 3 *facilitates* katika hizi Level 2 and 3 *facilitates* ni ile sehemu ambayo inatibu haya magonjwa kama *Flu...*

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Order! You are confusing me. Standing Order 73 (2), *A Member who begins a speech in any of the languages provided shall continue the same language until the conclusion of the Members speech*, so Honourable Ogutu speak one language.

**Hon. Ogutu:** Chair, can you read that Standing Order to totality.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): I have done that.

**Hon. Ogutu:** Because it gives a chance if you want to stress a point you can do it in another language Mr. Speaker.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): That is not provided in the Standing order so please just stick to one language.

**Hon. Ogutu:** *Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nafikiri*, I stand guided I was just saying that in each and every Sub County we will have at least one Level 4 facility then we will also have Level 2 and 3 facilities whereby in Level 1 and 2 they are treating diseases like flu and such likes, then we will have a Level 1 the community unit so in that line you will see that there is decongestion of Coast General. Then on the issue of the infrastructure we also recommended that most of the facilities are dilapidated and they are in bad state we recommended that there are supposed to be repaired immediately and on the issue of staffing we also said that from Level 2 to Level 5 which is Coast General there should be proper staffing so that people cannot just get access to quality health services but get access to quality health services. Another concern was on the issue off...

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Order Honourable Ogutu. Please advise me are you responding to a statement or you are contributing to this matter?

**Hon. Ogutu:** I am contributing to this Motion Mr. Speaker.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Okay please proceed.

**Hon. Ogutu:** Another concern was on the issue of land tenure; we found out that most of the facilities lacked title deeds and most of them were grabbed, so Mr. Speaker I can see the mover maybe wants to say something but...

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): What is your point of order.

**Hon. Katana:** Mr. Speaker I am standing on a Point of Order; I understand the Chair to Health Committee maybe brought in some report...

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Honourable Allen Katana, could you cite the Point of Order.

**Hon. Katana:** Okay, the point of order is; is the Honourable Member truly in order in giving the report to Motion or he supports the Motion I do not understand. Thank you.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Yes, Honourable Ogutu.

**Hon. Ogutu:** Mr. Speaker, I do not know whether the mover of this Motion understands his motion because he is talking about decongesting Coast general and the measures that am putting in place are aimed at decongesting the facility Mr. Speaker so maybe I stand guided if the Mover understands his Motion...

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Yes, Honourable Allen Katana?

**Hon. Katana:** Okay to my level of my understanding Honourable Speaker. The Honourable Member to stand and say to his opinion he thinks that if he takes these steps then we shall be doing greater and instead of him saying we, we, it is like giving us a report of whatever they did. Thank you.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Well noted Honourable Allen Katana. Yes, Honourable Benard Ogutu please be advised, you are not responding to a Statement or report when you say issues like we recommended, we did this I think you are not contributing to the Motion.

**Hon. Ogutu:** Chair I stand guided but I was responding to prayer number one and when I say we this is something that has been done and I think even the Motion is passed by events now that is on the floor, we will just contribute but again I just want to say it is a good Motion...

*[Applause]*

Because if anything done to make healthcare accessible I think that is very important on the issue of having facilities in every Ward I think this was well captured and we said that for every person to get accessed to quality health services without walking far distance we must have facilities at the Ward level and if possible for the start we said we could have well-structured containers to act as maybe facilities at those level at the time when we do not have enough funds to construct maybe a facility in the Ward. So, I think it is a good move and I congratulate the mover for it but again am advising him to read and understand that the report, Chair we should not take for granted anything that we pass in this Honourable House because the report was here, we read it and understood it and we passed it so the Mover should go back and read that report and understand it. Thank you, Mr. Speaker.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Well, noted. Yes, Honourable Milka?

**Hon. Ngare:** Thank you Mr. Speaker for giving me this chance to also contribute. I am up on a point of support for the Motion introduced to this House by the Chair Education Honourable Allen Katana. First, before I give my contribution, I want to repeat something that I said here yesterday; for a long time, we have been bringing such essential Motions to this House in fact there was almost a similar Motion introduced to this House but what happened is the implementation is the issue. Again, the backstops with the Chairperson of Implementation; I kindly request that Chair Implementation just go back to the archives of all the Motions that we have passed combine with this Motion brought by Honourable Katana plus the similar one that have been passed before then see how that can be implemented and this House would have done something...

*[Inaudible]*

The Motion introduced by Honourable Katana on the prayers that he has given I will agree with him 100 per cent that Coast General is indeed congested. I am a living example of having taken there, patients several times including my own relatives and it took me to introduce myself as an Honourable Member and a Member of Health Committee to be near getting a service! One day I stayed there the all day trying to have a patient treated; it was such a hectic task, so for the prayers he has given including Port Reitz upgraded is wonderful, having each Sub County a Level 5 facility already we have in Shanzu I think that Utange Health Facility which can be upgraded to a Level 5 and am sure if all the facilities are...

*[Inaudible]*

...It will be decongested and am very sure the Honourable Member seated next to me Honourable Ngugi would want in each Sub County a health facility to cater for the People living With Disabilities (PWDs) because all the PWDs are accessing the Coast General Level 5 is a nightmare for them. So, the prayers that Honourable Katana has brought in to this House are very valid and I support 100 per cent but that alone also when they are upgrading and the Governor maybe tries and get more resources. We also need more human resource; we need more doctors; we need more nursing staff so the hospitals are well equipped day and night. You should try and visit Coast General one of these fine days at night and you will come back a very disappointed person because services come to almost a standstill unless it is really an emergency and you have some power to push for services. So, I support the Motion by Honourable Katana 100 per cent and my Chairman of Health has highlighted that the taskforce is addressing most of these prayers that Honourable Katana has brought. We are hoping and wishing that taskforce report is put into use as soon as possible so that we do not see such kind of scenes at the Coast General Hospital. Thank you, Chairman Health for highlighting that and May God give you more wisdom to continue following up on matters of health. Thank you so much Mr. Speaker.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Thank you. Well noted. Honourable Mwaka Bakari?

**Hon. Mwaka Bakari:** Ahsante sana Bwana Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuweka sauti yangu kidogo kwenye Mswada huu. Nasimama kuiunga mkono kwa sababu, mimi kama mkaazi wa Likoni nina masikitiko makubwa sana...

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Yes, Honourable Ngugi?

**Hon. Ngugi:** Sio Bwana Mwenyekiti ni Mheshimiwa Spika. Ahsante.

**Hon. Mwaka Bakari:** Napenda kukurekebisha Bwana Mwenyekiti ni sawasawa na Bwana Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Yes, overruled. Proceed please.

**Hon. Mwaka Bakari:** Sawa sawa, Kiswahili sanifu hicho pia umeniregesha nyuma sana. Napenda kuunga mkono hoja hii kwa sababu, unajua kuunga mkono ni lazima inakugusa. Mimi nimeguswa kama mkaazi wa Likoni kwa sababu Likoni tuko na Zahanati mbili ambazo Zahanati moja ni Likoni Health Centre, moja ni Mrima, na Likoni Health Centre ni hospitali ambayo ni Mama wa Likoni tangu 1980's na mpaka sasa ukiangalia Zahanati ile inasikitisha, ikiweko Waheshimiwa wenzangu wanaweza kuniunga mkono vile ambavyo iko. Hata Mheshimiwa Juma Mwalimu alikuwa hajazaliwa nafikiri hio hospitali, hata Mheshimiwa Manuari hajazaliwa Hospitali ile. Ukiangalia Mheshimiwa Spika ni hospitali ambayo inasikitisha, mpaka kufikia sasa Zahanati ile ambayo kwamba inapokea wagonjwa wa Likoni hata wengine kutoka hata Kwale Kaunti jirani, lakini pindi utakapofika pale hakuna huduma ambazo zinatosheliza isipokuwa tuvuke. Bwana Spika na unajua kama kuvuka kwetu, pahali kuna msukumano, ukifika pale gari la ambulansi, meli zinapita mgonjwa yule yuwapata tabu. Tukienda hospitali nyengine ambayo ni ya Zahanati ya Mrima, vile vile Zahanati ya Mrima ilikuweko na mashirika, mashirika waliweza kutowezesha na yalivyoondoka mashirika hospitali ile haina sura. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mimi nasimama kuunga hoja hii ili iweze uzito na iweze kuleta uzito na iweze kufwatilizwa kama Mheshimiwa Milka alivyosema tunaweka hoja nyingi sana hapa lakini kufwatilizwa hakuna na wala utendaji kazi wa lile jambo lile huwa hakuna. Tunaongea kama nyimbo na tukitoka hapa tunawachia hapa. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika jambo la afya ni jambo muhimu sana nataka liwekwe mkazo na liweze kufwatilizwa ili iweze sura ya kuweza kusaidia wagonjwa wetu kule mashinani. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Yes, just for the record Honourable Ngugi I am the Chair of this session and I am also the Speaker of this House. Yes, Honourable Madialo please make your contribution.

**Hon. Madialo:** Thank you Mr. Speaker. From the onset I would like to support Honourable Katana's Motion...

*[Applause]*

But I would also like to advice the House, if the House Business Committee was keen, they would have not allowed prayer number one and prayer number three; they would have advised the mover of the Motion to bring prayer number two because all these things have been passed here barely a week ago when we adopted the report.

So, the reason why maybe sometimes we move Motions here and they are never taken seriously is because we throw a lot of papers in the air and that is why my Chairman for Health was finding a little bit hard to execute his points because when he was explaining you guys were thinking that he was responding to a statement. If we are keen, we will realize that, for example this prayer number one, *the County government through the Department of Health to conduct a strategic needs assessments survey of the infrastructure, equipment and human resource capacities of all Health facilities* and blah blah it goes on. Prayer number three, the same, all that was captured comprehensively. So, if I would have been asked it is the Port-Reitz Health facility when it was mentioned in the report, the recommendations were, that the mental side, mental unit be upgraded so maybe the only prayer here that is a bit different from that which was captured in the report is that Port-Reitz be upgraded to Level five of which I fully support. So, even as I support, I request that the House Business Committee should always be keen when recommending to the Motions that come to this House. I believe that there other Motions that are completely new that can enhance the business of the House which should be prioritized. So, Honourable Katana, I support this Motion but I would like to humbly inform you that all these things apart from Port-Reitz Level 4 being upgrades all of them are in that report and the Honourable Chair and the Speaker presiding over this session was there when we were giving the Governor that report and he said all these things he is going to implement. Thank you so much.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Well noted Honourable Madialo, your message will be conveyed to the House Business. Yes, Honourable Leila?

**Hon. Nyache:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi kuweza kuniona. Kwanza nimesimama kidete kuunga mkono hoja hii iliokuja na Mheshimiwa mwenza Bwana...

*[Interruption]*

Mheshimiwa Spika, nilinde hapa Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ananichokora chokora...

*[Laughter]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Yes, Honourable Ogutu, what is the matter? What is the issue Honourable Ogutu.

**Hon. Nyache:** Halloo!

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Ogutu, what is the issue?

**Hon. Ogutu:** Nilikuwa namuambia aunge mkono hiyo ya Port- Reitz maanake Port-Reitz iko Changamwe Mheshimiwa Spika.

**Hon. Nyache:** Ni muongo lakini wacha tumuache hivyo hivyo na tabia yake.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Okay proceed, proceed.



**Hon. Nyache:** Ahsante, ahsante Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunilinda. Kwanza naunga mkono hoja hii iliokuja na Mheshimiwa mwenza Mheshimiwa Katana; nasema hoja hii ni nzuri na pia itaweza kutuletea natija sisi Waheshimiwa wenye ambao hatuna mahospitali ama italeta natija katika jimbo letu la Mombasa. Kwanza kusema ya kuwa Makadara iweze kuwezesha, kuwezesha kwake ni hii hospitali ya Port-Reitz iweze kuwezesha ndio ule msongamano wa pale Makadara utaweza kupungua ndio kuwezesha kwa Makadara lakini bila kuwezesha hii Hospitali ya Port-Reitz kutakuwa ni vile vile. Kwa hivyo mimi naunga mkono kuwezesha hii Hospitali ya Port-Reitz, maanake sisi tunatoka sehemu ya Changamwe, mimi ninawakilisha wananchi wa Wadi ya Kipevu na kwangu pia hakuna zahanati Mheshimiwa Spika. Sasa mimi naunga mkono kama vile Mwenyekiti wa Afya alivyosema *Level 2, Level 3* zitakuwa ama *Level 1* katika kila Wadi itakuwa vizuri sana itaweza kusaidia watu wetu kupitia kutibiwa ama kupitia maradhi. Sisi kwanza Katika Wadi ya Kipevu tukipatwa na maradhi yoyoye tunaenda kwa Wadi ya Ogutu Changamwe, tunaenda Port-Reitz, tunaenda Wadi ya Chaani, vikizidi ndio tunaeleka Makadara. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, mimi ningeunga mkono Port-Reitz iweze kuwezesha na itaweza kutusaidia hasa sisi wakaazi wa Changamwe kwa sababu tunavuka kuja huku Makadara wakati gonjwa limekuwa limezidi ama gonjwa halisikii dawa tunatumwa huku Makadara. Hivyo basi mimi naunga mkono na pia naunga mkono kila Wadi ambayo haina Zahanati iweze kuwekewa hiyo *Level 2* mojawapo ikiwa ni Wadi ya Kipevu. Nikipata kama hiyo *Level 2* wananchi wangu wataweza kuwa na afya bora. Ahsante sana Mheshimiwa Spika na naunga mkono hoja hii.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Yes, thank you. Yes, Honourable Mariam Baimu.

**Hon. Baimu:** Kwanza ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii. Pili namuunga mkono Mheshimiwa Katana kwa hii hoja alioileta hapa mbele yetu; ni hoja kweli ya muhimu sana. Nikiongelea mimi ningependa kutia msisitizo sana hizo Wadi mbili; ambayo ni Shanzu na Port-Reitz kama zitaweza kupewa nguvu, zikawekewa madawa ama vifaa ambavyo vitasaidia ili huo msongamano ama watu kujaa hapo Coast General waweze kupungua. Mimi ningeomba pia hizi Wadi zetu kama mimi Frere Town na hizo Kliniki mbili hospitali ndogo kwa hio ningeomba pia kama twaweza kupata madawa pale ya kutosha na vifaa vya zamani viweze kurekebisha ili pia watu wetu wa Frere Town waweze kusaidika. La mwisho ningemuomba Mheshimiwa Katana hoja yake ya kusema kwamba wafanyakazi watoke tu sehemu ya kwake Shanzu; ningekuomba Mheshimiwa mwenzangu Frère Town iko karibu na kwako wagonjwa tukubalie waje kwako na hata kazi pia watu wangu wapate kwako. Ahsante sana.

**The Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Honourable Mwalimu karibu sana.

**Hon. Juma Mwalimu:** Ahsante sana Bwana Mwenye Kiti. Mimi nimesimama kuunga mkono hoja hii ya ndugu yangu Mheshimiwa Katana na kusema pia sisi kama Waheshimiwa katika ile Zahanati ya Coast General hua hatuheshimiki kabisa hata ukijitambulisha wale wahudumu ni kama ambae hawataki kujua wewe ni nani. Kwa hivyo hii hoja hii ikipitishwa ningeomba kupitia Mwenyekiti na pia kupitia Kamati ya Afya wapeleke hata kama ni majina yetu pale Coast General ili tukiwa na shida yoyote kwenda kusaidia watu wetu tuweze kutambulika na watu wetu wapate huduma pia bila shida, na vile vile pia nataka pia niseme kule kwetu Likoni kuna Hospitali ambazo Mstahiki Gavana Joho alizijenga lakini la kuhuzunisha saa hizi kuna Hospitali moja kule Shonda imekua ni jumba la kufugwa kuku.

Kwa hivyo tunaomba pia hiyo hospitali iweze kumalizwa na watu wa hiyo sehemu waweze kupata huduma kwa sababu miji inakua kila kitu bado kuwekwa milango lakini wale wanaofanya ulinzi pale waliamua pia kulifuga kuku hilo jumba. Hivyo basi naomba pia iweze kutimiza ili wakaazi wetu waweze kupata huduma. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipatia fursa hii.

**The Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Thank you. Yes, Honourable Eliud Kimari.

**Hon. Kimari:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nasimama kuunga mkono hii hoja ya Mheshimiwa GB moja ama Allen Katana katika jina lake rasmi. Mheshimiwa Spika ukiangalia hali ilivyo katika Wadi zetu hususan Wadi yenye nimetoka ya Mkomani hali ni mbovu, na jambo la kwanza tungesema hapa ningeanzia ni ile ukarabati wa zile *health facilities* zenye ziko kule mashinani. Ukiangalia kwa mfano Mkomani tuko na hospitali yenye inaitwa Maweni Dispensary, ile Maweni Dispensary hali yake ni duni kiangalia pale ukifika pale ndani Mheshimiwa Spika huwezi hudumiwa utakua *referred* Coast General Hospital kwa sababu kama tungeweza kukarabati hizo hospitali tungeweza ku *decongest*, tungeweza kupunguza wale watu wana kuja Makadara Hospital na ukiangalia hali ilivyo katika zile hospitali hata vitanda zenyewe hakuna, hata ukipata dharura hususan umekumbwa na ajali kule barabarani utapata hata ile huduma ya kwanza ni ngumu kupata pale Mashinani na inabidi tunaleta msongamano hapa Coast General Hospital. Kwa hivyo jambo la kwanza nikiunga hii hoja ya Mheshimiwa Katana ni turekebishe kwanza zile hospitali. Hiyo ingekua hatua ya kwanza...

[Applause]

...Tuweze kuzirekebisha kama ni madawa ziwe na madawa kwa sababu kuna yale magonjwa madogo madogo yanayotakiwa kutibiwa katika zile hospitali yalishinda hizo hospitali ndiyo tunaleta Makadara lakini utapata hata mtu ameumwa na kichwa pale mtaani lakini anakuja wapi, anakuja Makadara. Vilevile ukifika Makadara Mheshimiwa Spika, mimi nimepatana na jamaa zangu wengine lakini wamepata ajali huku barabarani wanaenda Makadara ukifika pale Makadara hususan kwa sehemu ya dharura utapata mtu amekuja pale anatoka damu amepata ajali kule barabarani lakini hata kutibiwa anachukua saa moja kabla hata apate hata yule mtu wa kumshughulikia. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika hili swala linataka kutiliwa mkazo na vilevile hata kupunguza watu wanaoenda pale Makadara ama Coast General Hospital kuna ile tunaita *mobile Clinics* zile *mobile Clinics* pia zinaweza changia kupunguza wale watu wanaokuja pale Makadara kama zinaweza kuwekwa kama zitakuwa zinafanya katika awamu tofauti tofauti katika Wadi zinaenda kwa mfano; inaenda Mkomani, inaenda Old Town hata itaweza kupunguza ule msongamano wa pale Makadara. Kwa hivyo nashukuru, nashukuru Mheshimiwa Katana na nikimalizia nataka kumwambia Mheshimiwa Katana si lazima wafanyaji kazi wote asilimia mia kwa mia watoke Shanzu, hata wagonjwa watatoka pale na watakuja kutibiwa. Mgonjwa wa kutoka kwake atakuja atibiwe pale Maweni Dispensary si lazima atoke hapo aende atibiwe wapi aende atibiwe kule kwake na vile vile hata wafanyikazi si lazima watoke asilimia 100 wawe wanatoka kule, hiyo atakuwa anaenda kinyume...

[Applause]

...atakuwa anaenda Kinyume na *Article 27* ya Katiba ambayo inazungumzia kuhusu mambo na usawa. Ahsante.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Thank you, now may I ask Honourable Katana to respond to the Motion bearing in mind the sentiments and the inputs of all the Members, please respond.

**Hon. Katana:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii na nawashukuru Waheshimiwa wote waliotoa changizo zao na katika hoja hii na kwa ruhsa yako ningewataja kila mtu tofauti na maneno waliyosema lakini maneno waliyosema Waheshimiwa hawa hayana tofauti kwa sababu wengi nawaunga mkono swala hili. Utofauti kidogo unatoka kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Leba na Mheshimiwa Mwenyekiti wa mambo ya Afya lakini pia niwakumbushe Bunge hili tumelikuta na tutaliwacha na Bunge hili halitaleta mambo mapya zaidi ya yale yale ya kumtetea mwananchi kila uchao. Nitaje maneno ambayo Mheshimiwa ambaye nina muheshimu sana; Mheshimiwa Milka ya kuhimiza Kamati tekelezi inayoongozwa na Mheshimiwa Mwenyekiti Mheshimiwa wa Kongowea ya kwamba haya mambo tunayo yaongea hapa ama tunayowasilisha katika Bunge letu tukufu hili ni kwamba itakuwa bora zaidi mambo haya kama yatatendeka.

Mheshimiwa Spika lakini swala la kusema kwamba haya yalinenwa tayari kwa hivyo hayastahili kunenwa, Mheshimiwa Spika kwa hakika ya kwamba miaka ya nyuma sikuwa kwa Bunge hili, hamna mapya walioongea tofauti na haya tunayoongea. Kitu tunachofanya Mheshimiwa Spika ni kukumbushana na kusesitiza ili mwisho wa kwisha Mheshimiwa Spika tuhakikishe maisha ya watu wetu yanapata mabadiliko. Kitu chengine ambacho nitakisema Mheshimiwa Spika ni kile Mheshimiwa Kimari alichokisema ya kwamba wafanyikazi wawe watatoka sehemu nyengine nyengine lakini kuna kipengele kingine ambacho utanisamehe kwa sana nimekisahau kinachosema asilimia 70 ya watu watokee maeneo yale. Kwa hivyo nitawaruhusu Mheshimiwa Mariam Baimu na Mheshimiwa Kimari kwa ile thelathini mutagaanyizana nyinyi. Kitu chengine ambacho sitaki kusahau Mheshimiwa Spika ni kumpongeza Mheshimiwa Kimari kwa kumaliza kesi yake kortini jana. Kwa hayo nasema ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdulkadir): Thank you. Honourable Members, I now put the question that this House adopts the Motion by Honourable Allen Katana on measures to decongest Coast General Teaching and referral Hospital to be considered by this Honourable House in the same, to be adopted by this Honourable House. Am repeating again, I now put the question that this House adopts the Motion by Honourable Allen Katana on measures to decongest Coast Teaching and referral Hospital to be adopted by this Honourable House in the same terms as moved?

*[Question put and agreed to]*

Yes Clerk?

## MOTION

APPROVAL OF THE COUNTY ASSEMBLY CALENDAR SECOND SESSION

Just a communication from the Speaker that the Motion on approval of the County Assembly calendar second session was to be moved by the Majority Leader Honourable Athman Mwamwiri. I understand he is not present and as such I can also see that no Member of the House Business Committee is here to move this Motion so this Motion will be deferred back to the House Business or rather will be deferred in the House in the afternoon so be guided Members. Yes Clerk?

### **ADJOURNMENT**

Honourable Members this House remains adjourned until Wednesday at 2:00p.m.

The House rose at 11:23a.m.